**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI**

**MKUU – TAMISEMI**


**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0745573360**

**Makamu Mkuu wa Shule:- 0744356478/ 0755253551**

**Matron:- 0742772660**

**Shule ya Sekondari Nyantakara,**

**S.L.P.182,**


**Tarehe 14/05/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P……………………………………..**
**…………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NYANTAKARA HALMASHAURI YA BIHARAMULO MKOA KAGERA MWAKA ………….**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……….. na atasoma tahasusi ya ………….

   Shule ya Sekondari NYANTAKARA ipo umbali wa Kilometa 73 Mashariki mwa Mji wa BIHARAMULO. Usafiri wa basi kutoka mjini BIHARAMULO hadi Nyantakara shuleni ni shilingi 9000/=. Kutoka kituo cha mabasi RUNZEWE- BUKOMBE hadi Nyantakara shuleni nauli ni Shilingi 3,000/=

   Muhula wa Masomo utaanza ………., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni mara tu Serikali itakapotangaza tarehe ya kuripoti. Mwisho wa kuripoti shuleni itakuwa baada ya wiki mbili tangu tarehe ya kuripoti kutangazwa.

1.1 **Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii ni shati 2 nyeupe mikono mirefu na sketi 2 rangi ya dark blue kwa ajili ya darasani, Mshono:- (Linda box kubwa moja mbele, kubwa moja nyuma na manne (4) madogomadogo kushoto na kulia ) iguse kisigino.
ii. Rangi ya Hijab (kijuba) ifanane na shati ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iii. Sare ya Michezo ni track suit rangi ya blue tu na raba rangi yoyote.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi/stocking jozi mbili nyeupe za shule.
vi. Sweta 1 rangi ya kijivu iwe na nembo ya shule.
vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) gauni 1 rangi ya Pink rose iwe ndefu iguse kisigino yenye mshono wa solo, sketi rangi ya kijani jeshi iguse kisigino, Tshirt rangi ya maruni yenye kola isiwe na maandishi. Iwe na nembo ya shule
viii. Tisheti 1 ya shule Rangi ya dhahabu (gold) iwe na nembo ya shule.

NB: **Sketi mbili dark blue za darasani, sketi ya kijani jeshi, gauni rangi ya pink rose, hijabu (kijuba) na Tshirt rangi ya gold ya shule vinapatikana shuleni. Fuata maelekezo ya sare ya shule ili kuondokana na gharama za kununua mara mbili. SIKU YA KURIPOTI MWANAFUNZI AJE AMEVAA TRACK SUIT YA BLUE YA SHULE. PIA WANAFUNZI WA KIISLAMU WAWE NA MAJUBA YA KUSHINDIA KUENDANA NA RANGI ZA NGUO ZAO ZA KUSHINDIA NA SIO MITANDIO.**

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari (Counterbook Q3) – 10
ii. **Ream (A4-DOUBLE A)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka na graph pad mbili kwa mwaka kwa kila mwanafunzi.
iii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
iv. Original Scientific Calculator kwa michepuo ya PCM, PCB na CBG
v. Godoro kwa wanafunzi wa Bweni liwe na vipimo vya Ft 3X6 . Mashuka Jozi 2 rangi ya pink na blue, blanket 1, foronya ya mto 1 na chandarua 1.
vi. Nguo za ndani za kutosha;
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 (Lita 20 moja na lita 10 moja zenye mifuniko)
ix. Mchepuo wa PCM walete Kwanja 1 na fagio ya nje1 na reki moja, Mchepuo wa PCB walete kwanja 1, mopping rubber 1 na mfagio wa ndani mmoja (soft broom). Mchepuo wa CBG walete jembe na mpini 1 na mfagio mgumu 1 (hard broom).
x. Kila Mwanafunzi aje na copy ya vyeti vya taaluma na cheti cha kuzaliwa.
xi. Mwanafunzi aje na laboratory coat kwa michepuo yote.
xii. Tochi ya betri/solata kwajili ya matumizi yao binafsi endapo umeme utakata, toilet paper za kutosha kwa matumizi binafsi na sanduku imara la kutunzia vifaa vya mwanafunzi (tranka).

**1.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango yote ya Shule ilipwe kwenye AKAUNTI YA SHULE 31701200086- NYANTAKARA SECONDARY NMB BANK.**

- **Mwanafunzi LAZIMA aje na BIMA YA AFYA YA NHIF AU ALIPE 50,400/= KWENYE AKAUNTI YA SHULE 31701200086 – NYANTAKARA SECONDARY katika Benki ya NMB NA MWANAFUNZI AJE NA PAYSLIP YA BANK KWA AJILI YA KUKATIWA BIMA SHULENI.**
- **ANGALIZO: Pesa Taslimu haitapokelewa shuleni.**

## 2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

## 2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu.
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 2.3 Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**FOMU YA KUANDIKISHWA SHULE**

**(ijazwe kwa herufi kubwa na irejeshwe kwa mkuu wa shule)**

1. Jina kamili
…………………………………………………………………………………………………….

Tarehe ya kuzaliwa………………….. Wilaya …………………..Mkoa…………………………..

Taifa ………….Dini:RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecoste/ nk…........................Shule ya sekondari unayotoka………………………………………………………..

2. Jina la Baba/Mama/Mlezi………………………………………………………………… Anwani yake ...................................................................................................... Kazi ya Baba/Mama/Mlezi.........................................................................................Namba ya simu ……………………………………………………………………………

**3. AHADI YA MWANAFUNZI**

(a) Mimi...................................... nimeyasoma na kuyaelewa yote ambayo ni pamoja na sheria ya kanuni za shule na nimekubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Nyantakara kuanzia tarehe....................................hadi nitakapomaliza kidato cha sita.

(b) Kwa hiyo naahidi kwamba:-

i. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa

ii. Sitashiriki vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa serikali ya jamhuri ya m

iii. Muungano wa Tanzania.

iii. Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na majengo, samani, vitabu n.k.

Tarehe…………………………… sahihi ya mwanafunzi………………………………………

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**SHULE YA SEKONDARI NYANTAKARA,**
**S.L.P 182,**
**BIHARAMULO.**
**…………………**

**FOMU**

MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA/KITUO CHA AFYA

Jina........................................................................................ amechaguliwa kujiunga na kidato cha......... katika shule hii, kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza. Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona macho yake. Kama imeshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha yake.

Tafadhari nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kumpima.

Ahsante kwa ushirikiano

……………….
**Asimwe S . Bora**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI…………………….
S.L.P………
**BIHARAMULO**

Nimepima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu nakuona kwamba ana matatizo/ugonjwa wa;

A. Kifua kikuu……………………………………………………………………………..
B. Macho ……………………………………………………………………………………
C. Masikio ………………………………………………………………………………….
D. Akili………………………………………………………………………………………
E. Kilema chochote ……………………………………………………………………..
F. Choo ……………………………………………………………………………………..
G. Kwa wasichana tu nimeona/hana mimba………………………………………..
H. Mengineyo……………………………………………………………………………….

**SAINI MHURI WA OFISI…………………………………………………………..**

**MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA/KITUO CHA AFYA…………………………………**

**AHADI YA MZAZI /MLEZI**

Mimi ...................................................... Ambaye ni mzazi/mlezi wa

Mwanafunzi.........................................................ninahaidi kwamba

1. Nitashirikiana na uongozi wa shule, walimu na watumishi wasio walimu katika kuhakikisha mwanangu, wanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Nyantakara na iwapo atashindwa kutii sheria hizo, nitalazimika kumuondoa katika bweni.
2. Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanafunzi kusoma kwa kulipa michango ya shule na mingine kama ilivyoelekezwa na shule.

Tarehe …………………………………………………………………………

Sahihi ………………………………. Namba ya simu………………………..

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ……………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …** A S I M W E S. BORA

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………………..**

HEADMISTRESS
NYANTAKARA SECONDARY SCHOOL
BOX 182 BIHARAMULO

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

**i.** **Mkuu wa shule : 0745 57 33 60**
**ii.** **Makamu Mkuu wa Shule : 0744 35 64 78/ 0755253551**
**iii.** **Mwandamizi Taaluma : 0757 710 199**
**iv.** **Mwandamizi Malezi : 0758 39 82 83**